# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA BOHARI KUU YA DAWA ZANZIBAR KWA AJILI YA UNUNUZI, UTENGENEZAJI, UHIFADHI NA USAMBAZAJI WA DAWA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.

---

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyetujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako Tukufu kuendelea na majukumu yetu ya Kitaifa.

Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niwasilishe maoni kuhusiana na “***Mswada wa Sheria ya kuanzisha Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar kwa ajili ya Ununuzi, Utengenezaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa na Mambo mengine Yanayohusiana na Hayo***”, kwa niaba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa ujasiri wake katika jukumu zima la uongozi wa nchi hii

sambamba na jitihada anazochukua za kuendeleza sekta ya Afya hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba pia nichukue fursa hii kuipongeza Timu ya Wataalamu ya Wizara ya Afya kwa mashirikiano yao waliyoipatia Kamati yetu katika kipindi chote cha majadiliano ya Mswada huu.

Aidha, napenda kuwashukuru Wanasheria wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uchambuzi na ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu katika hatua ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** pia nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kazi nzito waliyoifanya ya kuujadili na kuuchambua Mswada ulioletwa mbele yao kwa upeo na hatimae kutoa maoni. Naomba sasa niwatambue Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii mmoja baada ya mwengine kama ifuatavyo:

| NA. | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | MHE. SABIHA FILFIL THANI | Mwenyekiti |
| 2 | MHE. NASSOR SALIM ALI | M/Mwenyekiti |
| 3. | MHE. SULUBU KIDONGO AMOUR | Mjumbe |
| 4. | MHE. BIHINDI HAMAD KHAMIS | Mjumbe |
| 5. | MHE. ABDALLA HUSSEIN KOMBO | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | MHE. SALMA MUSSA BILAL | Mjumbe |
| 7. | MHE. HAJI OMAR KHEIR | Mjumbe |
| 8. | MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika, p**ia niwatambue Makatibu wetu wa Kamati ambao wamekuwa wakitusaidia katika kutekeleza majukumu yetu ipasavyo, kama ifuatavyo;

1. Nd. TALIB ENZI TALIB Katibu
2. Nd. SALHA ABDULLA ABDULLA Katibu na
3. Nd. BAKAR MAKAME HAJI Katibu

**Mheshimiwa Spika,** *Fasili ndogo ya 7 ya Kanuni ya 84 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020* inaipa uwezo Kamati kuwaalika Wadau mbali mbali kila inapotokea kazi ya kujadili Miswada ya Sheria.

Kamati inathamini mchango mkubwa wa Wadau hao na inawashukuru kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kutambua nafasi yao katika utekelezaji wa Sheria ya Wakala wa Bohari itakayoanzishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Uimarishaji wa Sekta ya Afya ni kipaumbele moja wapo cha Serikali ya Awamu ya Nane ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa huduma ya dawa salama zinapatikana kwa wananchi wote. Kamati yetu inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuleta Mswada huu sambamba na uwanzishwaji wa Mfuko wa Bima ya Afya, matarajio ya Kamati ni kuona huduma ya upatikanaji wa dawa inawafikia wananchi kwa

ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** kimsingi, Kamati yetu inakubaliana na dhana nzima iliyobebwa na Mswada huu. Kamati ilipendekeza marekebisho mbali mbali wakati ilipokaa na Wizara kwa nia ya kuwa na Sheria itayoleta ufanisi katika utekelezaji wake. Marekebisho hayo yalijitokeza katika sehemu mbali mbali zikiwemo makosa ya kiuandishi, makosa katika uteuzi wa maneno, kuingiza baadhi ya maneno pamoja na vifungu vipya.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na Kamati kukubaliana na dhana nzima iliyobebwa na Mswada huu, bado Kamati inaishauri Serikali kuipa Wakala wa Bohari hadhi ya ***Kampuni*** ili taasisi hiyo iweze kujitegemea na kufanya kazi kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Baadhi ya sababu za msingi za maoni ya Kamati kuwa Wakala kupewa hadhi ya kuwa ***Kampuni*** itakayojitegemea ni kama ifuatavyo:

**Kwanza**, uzoefu unaonyesha kwamba Wakala wengi walioanzishwa Zanzibar, Mfano; Wakala wa Barabara, Wakala wa Uchapaji wanashindwa kufikia lengo katika kutekeleza kazi zao kutokana na urasimu wa upatikanaji wa fedha.

**Pili**, Kufuatia Utafiti uliofanywa na kwa kufuata uzoefu wa nchi zinazofanya masuala kama haya ya Uwakala wa Dawa,wamebadili mtazamo na kuwa na Mfumo wa uwendeshaji wa **KAMPUNI** inayojitegemea badala ya kutegemea Serikali.

**Tatu**, Serikali itenge fedha za Mtaji kuwapatia Wakala kiasi cha Dola za kimarekani milioni 1.5 na iwapatie Hadidu Rejea za uendeshaji na kuwataka

Wakala kufanya biashara na kutoa gawio Serikalini.

**Nne,** Wakala upewe uhuru wa kibiashara ili uweze kuingia katika soko na kufanya kazi kwa ushindani.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza maoni ya jumla na ya msingi ya Kamati kuhusu Mswada wa Sheria ya kuanzisha Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar, sasa naomba niende kwenye baadhi ya vifungu ambavyo Kamati imeona vinahitaji marekebisho na marekebisho zaidi ya vifungu yanaonekana katika Waraka wa Marekebisho ambao wamepatiwa Waheshimiwa Wajumbe .

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imependekeza kurekebishwa Kifungu cha 3 kama ifuatavyo:

I. Tafsiri ya neno ''**Dawa**'' inarekebishwa kwa kufutwa neno ''**vinachokusudiwa** '' na kuwekwa badala yake neno ''**vinavyokusudiwa**''.

II. Tafsiri ya neno **''Ghala ya Dawa** '' pia inafutwa na kuachwa tafsri ya neno ''**Bohari**'' kwa vile zinaonekana kufanana.

III. Tafsiri ya neno ''**Wakala**'' inarekebishwa kwa kuingizwa neno ''**Zanzibar**'' baina ya neno ''**Dawa**'' na ''**ulioanzishwa**''

**Mheshimiwa Spika,** Aidha Kamati imependekeza kuongezwa kifungu kidogo kipya cha **4(2)(a)** na kisomeke; "**kushtaki au kushtakiwa**" na kufutwa maneno "**kwa mujibu wa sheria"**katika kifungu cha **4(2)(d)**

Kamati imependekeza kurekebishwa kifungu cha **5(2)** kwa kufutwa neno "**waraka**" na kuingizwa neno "**nyaraka yeyote**" baina ya neno ''**katika**'' na

‘’**yatathibitishwa**’’.

**Mheshimiwa Spika,** kwa vile kazi ya Wakala kwa mujibu wa malengo ya Mswada huu ni pamoja na kuuza Dawa kwa Mpewa Huduma hivyo Kamati imependekeza kurekebishwa Kifungu cha 7(1)(a) kinachoainisha kazi hizo kwa kuongezwa neno “**kuuza**” baina ya neno **“kununua**” na “**kuhifadhi**” ili lengo hilo liweze kufikiwa.

Kamati katika kubaini kuwa, kuwepo kwa kifungu cha7(1)(c) katika Mswada huu, kunaweza kuleta mgongano wa kimajukumu baina ya Wakala wa Dawa, Chakula na Vipodozi na Wakala wa Bohari. Hivyo Kamati imependekeza katika kifungu hicho kuongezwa maneno “**bila ya kuathiri Sheria nyengine yeyote**”

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imezingatia sifa za Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala ambapo imependekeza kuongezwa aya mpya ya (a) katika kifungu cha **10** itakayosomeka **‘’ sifa ya Uzanzibari”.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu pia imebaini makosa madogo madogo na imependekeza marekebisho ya makosa ya kisarufi na kuweka uwiano baina ya Mswada wa Kiingereza na Kiswahili.

Hata hivyo, Kamati imependekeza kufutwa kwa Kifungu cha **26(2)** ili Wakala afanye kazi ipasavyo na aweze kujitegemea.

**Mheshimiwa Spika,** napenda nimalizie kwa kuishauri Wizara kwa vile kumekuwa na vifungu kadhaa vinavyohitaji uwepo wa Kanuni, Kamati inashauri kuharakisha uundwaji wa Kanuni hizo mapema ili kuviwezesha vifungu vya Sheria kuweza kutekelezeka.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho niwashukuru Wajumbe wote kwa utulivu wenu katika kupokea maoni ya Kamati ya Ustawi wa jamii. Hivyo naomba sasa tuuchangie, tuujadili, tutowe mapendekezo na hatimae tuupitishe Mswada wa Sheria ya kuanzisha Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar kwa ajili ya Ununuzi, Utengenezaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa na Mambo mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………………

Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Ustawi wa Jamii,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**